***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Siku ___1___ ya kufungua shule ___2___ tumeingojea kwa hamu na ___3___. ___4___ asubuhi na mapema kisha nikaingia ___5___. Nilioga kwa maji fufutende halafu nikavaa ___6___ zangu mpya. Baada ya kula ___7___, niliingia ndani ya basi la shule na ___8___. Ndani ya basi mlikuwa na wanafunzi wenzangu ambao tulisalimiana ___9___ furaha. Tulipofika shuleni ___10___, tulishuka na kuingia madarasani.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. huo | B. hiyo | C. hizo | D. hilo |
| **2.** | A. ulikuwa | B. tulikua | C. ilikuwa | D. tulikuwa |
| **3.** | A. ghamu | B. gamu | C. shaka | D. hamamu |
| **4.** | A. Niliamuka | B. Nilidamka | C. Niliamua | D. Nilidemka |
| **5.** | A. hamumuni | B. hamamu | C. hamamuni | D. hamumu |
| **6.** | A. jezi | B. rinda | C. fulana | D. sare |
| **7.** | A. chajio | B. kishuka | C. kiamshakinywa | D. chamcha |
| **8.** | A. kutia nanga | B. kufa moyo | C. kung'oa nanga | D. kula mwande |
| **9.** | A. kwa | B. na | C. kwenye | D. katika |
| **10.** | A. petu | B. yetu | C. zetu | D. wetu |

Masomo ___11___ umuhimu ___12___ sana katika maisha yetu. Kila mtoto ___13___ kupelekwa shuleni ___14___ apate elimu. Elimu ndiyo inayotuwezesha kuwa na maisha bora ya ___15___. Sote tusome kwa bidii ndipo tufaulu maishani.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | A. una | B. zina | C. ina | D. yana |
| **12.** | A. kubwa | B. nyingi | C. mingi | D. mkubwa |
| **13.** | A. wanafaa | B. anafaa | C. wanafai | D. anavaa |
| **14.** | A. ina | B. ili | C. wala | D. lakini |
| **15.** | A. kuja | B. kisogoni | C. usoni | D. yaliyopita |

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Chagua sentensi ambayo ni sahihi kati ya hizi.
A. Nyumba ingine itajengwa pale.
B. Kalamu chochote kitamsaidia mwanafunzi.
C. Chupa chake kimejaa maji.
D. Mvua ya masika imeanza kunyesha.

**17.** Tambua sentensi ambayo imetumia kivumishi cha idadi.
A. Darasa hili litaoshwa na wanafunzi wale.
B. Wanyama wengi wanaishi msituni.
C. Nguo nzuri itapelekewa nyanya.
D. Viatu vingine vitaoshwa.

**18.** Chagua wingi wa:
**Uyoga wa mama ni mtamu.**
A. Yoga za akina mama ni tamu.
B. Uyoga wa wamama ni mtatu.
C. Yoga za wamama ni tamu.
D. Uyoga wa akina mama ni mtamu.

**19.** Kitenzi **songa** katika kauli ya kutendewa ni;
A. songea B. songwa
C. songewa D. songesha

**20.** Chagua ukanusho wa: **Mti ule umepandwa.**
A. Mti ule haujapandwa.
B. Mtu ule hukupandwa.
C. Mti ule hujapandwa.
D. Mti ule haukupandwa.

**21.** Salamu gani ambazo hutumika wakati wa asubuhi pekee?
A. Masalheri B. Sabalheri
C. Umeshindaje D. Alamsiki

**22.** 'Karibu nyumbani mgeni wetu'. Neno **karibu** limetumika katika sentensi hii kuonyesha;
A. maagano B. nusura
C. makaribisho D. umbali

**23.** Ikiwa jana ilikuwa Jumatatu, kesho itakuwa;
A. Jumanne B. Alhamisi
C. Jumatano D. Jumapili

**24.** Tumia **'ndi-'** kwa usahihi kujazia pengo.
**Chakula hiki ___________ cha bawabu.**
A. ndiko B. ndio
C. ndivyo D. ndicho

**25.** Teua sentensi ambayo imetumia tanakali ya sauti iliyo sahihi.
A. Barabara ya kwenda nyumbani imenyooka twaa!
B. Jiwe lilianguka majini tapwi!
C. Sarafu ilianguka sakafuni pu!
D. Maji yalidondoka tiriri!

**26.** Tambua arodha iliyo na majina ya ngeli ya **U - ZI** pekee.
A. nyumba, nyasi, nyama.
B. nyasi, mbao, ndevu.
C. ndizi, ndoano, ndevu.
D. mbuzi, mbao, nyimbo.

**27.** **"Tabia za mtoto hutegemea jinsi tabia za mzazi zilivyo."** Chagua methali inayorejelea maelezo haya.
A. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.
B. Uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi.
C. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
D. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

**28.** Sentensi gani iliyotumia **'ki'** kuonyesha namna?
A. Alikuwa akitembea haraka sana.
B. Kitoto hiki kina njaa.
C. Wacha kuongea kijinga.
D. Ukiniita nitaitika.

**29.** Shinda ni kukaa mahali mchana wote. Shinda pia ni;
A. matatizo au taabu
B. kuwa wa kwanza katika mashindano
C. kaa usiku wote bila kulala
D. weka mbegu ardhini na kuzifunika.

**30.** Ni orodha gani inayoonyesha aina zote za maneno katika sentensi hii?
**Mtoto yule anapika chakula.**
A. nomino, kivumishi, kitenzi, kielezi.
B. nomino, kionyeshi, kitenzi, kivumishi.
C. nomino, kivumishi, kitenzi, nomino.
D. kitenzi, kiashiria, kitenzi, nomino.

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Wanyama wamegawanyika katika makundi wawili; wanyama wanaofugwa nyumbani na wanyama wa porini. Wanyama wanaofugwa nyumbani ni kama vile punda, mbuzi, kondoo, mbwa na kadhalika. Wanyama wa mwitu nao ni kama vile simba, ndovu, chui, pundamilia na wengineo. Wanyama wa porini wana faida kubwa kwetu sisi wakenya. Wanyama hawa wa porini huhifadhiwa katika mbuga za wanyama. Hapo ndipo utakapopata wanyama mbalimbali. Wanyama wenyewe wana faida kama vile kuwavutia watalii. Watalii ni watu ambao huenda katika mbuga za wanyama kujionea wanyama hao. Faida ambayo watalii hutuletea ni fedha za kigeni. Wao hulipa kiasi fulani cha pesa kabla ya kuwatazama wanyama hao.

Faida nyingine ni kuwa wanyama wa porini wamesaidia watu wengi sana kupata kazi. Kuna watu ambao wameajiriwa kuwalinda wanyama hao. Pia kuna madereva wa magari ambayo huwasafirisha watalii wanapokuja kuwaona wanyama. Isitoshe, watalii hao huishi katika hoteli ambazo huwapa watu kazi ya kuwahudumia. Kwa namna hii, kiwango cha umaskini kinarudi chini kwa kuwa watu hao hulipwa mshahara baada ya kazi.

Umuhimu mwingine wa wanyama wa porini ni kuwa wamesaidia sana katika utengenezaji wa barabara. Ili magari ya watalii yapite bila tatizo lolote, barabara katika maeneo yaliyo na mbuga za wanyama huwa nzuri. Hili lina faida hata kwa watu wanaoishi katika maeneo hayo. Kwa sababu ya faida hizi na nyingine nyingi, ni vyema tuwalinde wanyama wa porini dhidi ya wawindaji haramu. Wawindaji hao haramu huitwa **majangili**.

Majangili huongozwa na tamaa na kujipenda. Bila shaka, wao huwa na **tamaa kama fisi**. Kila unapogundua kuwa kuna jangili mahali popote unashauriwa kupiga ripoti kwa maafisa wa polisi ili uchunguzi uanze kufanywa mara moja. Inapobainika kuwa watu hao huufanya uhalifu huo, wanafaa **kutiwa mbaroni** mara moja na kufunguliwa mashtaka.

Tatizo jingine ambalo linatishia kuwaangamiza wanyamapori ni moto. Kuna wakati ambapo moto huzuka katika misitu na kuwaua wanyama wa porini. Mara nyingi moto kama huo huanzishwa na wanaochoma makaa au wale wanaorina asali. Tunaiomba serikali kuhakikisha kuwa shughuli kama hizo zinazosababisha harasa kwa wanyama haziendelezwi hata kidogo. Kwa namna hii, wanyama hawa wa porini watakuwa salama na wataendelea kutufaidi.

31. Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kuwa;
A. kondoo, pundamilia na mbwa ni mifano ya wanyama wanaofugwa nyumbani
B. faida nyingi tunazopata huletwa na wanyama wakubwa
C. mbuga ya wanyama ni mahali ambapo wanyama kama vile farasi na paka hupatikana
D. watalii huja katika nchi yetu ili kujionea wanyama wa porini.

32. Kifungu hiki kinaeleza kuwa watalii;
A. huwa hawana jambo jingine la kufanya kule kwao
B. hulipa pesa za kigeni ambazo hazina faida yoyote kwetu
C. wana umuhimu kwa nchi yetu kwa sababu ya pesa ambazo wao hulipa
D. hushirikiana sana na majangili hapa nchini

33. **Si** kweli kuwa kupitia shughuli za watalii;
A. watu wengi wamepata kazi
B. kiwango cha umaskini kimerudi chini
C. barabara zimekuwa mbovu
D. nchi yetu imepata faida.

34. **'Majangili'** ni akina nani kulingana na ufahamu?
A. Watu haramu wanaoishi porini.
B. Wawindaji ambao hawana ruhusa ya kuwinda wanyamapori.
C. Askari ambao huwatafuta wawindaji haramu.
D. Watu ambao huwashtaki wawindaji.

35. Ufahamu huu unaonyesha kuwa majangili huongozwa na;
A. kujipenda na tamaa.
B. tamaa na umaskini.
C. tamaa na kuwapenda wanyama.
D. umaskini na kutosoma.

36. Maneno, **'tamaa kama fisi'** ni mfano wa;
A. tashbihi B. istiara
C. tanakali ya sauti D. nahau

37. Mwandishi anashauri kuwa majangili wanapogundulika mahali popote, tufanye nini?
A. Tuwashike.
B. Tuwapigie kwa polisi.
C. Tuwaambie maafisa wa polisi.
D. Tuwafukuze.

38. Wafuatao ni watu ambao ni hatari kwa wanyamapori **isipokuwa**;
A. majangili
B. wanaochoma makaa
C. wanaorina asali
D. magaidi.

39. Maneno **'kutia mbaroni'** yana maana gani jinsi yalivyotumiwa katika kifungu?
A. Kufungwa jela.
B. Kupiga ripoti kwa polisi.
C. Kushikwa na polisi.
D. Kushauriwa

40. Makala haya yanaeleza kuwa wanyamapori huwafaidi;
A. maafisa wa polisi pekee
B. Wakenya wote
C. maafisa wa serikali pekee
D. watalii pekee.

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.</u>***

Adhuhuri moja ya siku za mwishomwisho za mwaka, nilitoka kazini kabla ya muda wa kawaida ili kuyakimbiza mambo kadhaa. Nilienda katika mtaa wa Huruma kabla ya kupitia katika jiji kuu. Baada ya harakati tumbi nzima; kelele za wachuuzi, purukushani za utingo walioyanadi magari yao, kupishana na magari hapa na pale, niliingia ndani ya matwana moja na kutulia. **Usingizi ulianza kunibembeleza ili unifunike gubigubi**. Juhudi zangu zilivurugwa na sauti ya abiria mmoja aliyeingia ndani ya gari huku akiongea kwa sauti ya kuzua huzuni na huruma. Alirai kuwa aruhusiwe kukaa kwenye kiti kilichokuwa karibu na mlango. Alizungumza kwa kusitasita na usumbufu mkubwa.

Hata hivyo, kondakta alimhakikishia kuwa alihitajika kulipa nauli licha ya udhaifu wake. Baada ya matwana kung'oa nanga, jamaa yule aliyeingia ndani ya gari alisimama akaanza kuomba hela kutoka kwa abiria wengine. Kwa kuwa alielezea matatizo chungu nzima yaliyomkumba, watu walimchangia pesa bila tatizo lolote. Alidai kuwa alikuwa na mtoto mchanga kule nyumbani kwake ambaye alihitaji chakula na mavazi. Alipomaliza kukusanya pesa, takriban shilingi mia tano pesa taslimu, aliketi palepale alipokuwa awali na kutulia. Gari liliendelea kubugunya masafa kwa kasi.

Mara jamaa yule aliwashangaza wengi kwa kuitoa simu yake na kubofya nambari kadhaa. Ghafla alianza kuzungumza na mtu ambaye alimfurahisha na kumchekesha kwelikweli. Ajabu! Yaani mtu ambaye hakuwa na uwezo wa kumnunulia mwanawe chakula na mavazi ana simu! Hili lilishangaza si haba. Lile lililonishangaza zaidi ni kuwa sauti hiyo niliijua vizuri sana. Sasa hakuwa akiongea kwa kusitasita alivyofanya akiingia garini. Bila shaka! Huyo alikuwa Potoka. Potoka hakuwa tu jirani pale mtaani bali pia mwanafunzi niliyesoma naye hadi katika darasa la saba. Pale

mtaani aliishi katika kijumba kilichokuwa karibu kuanguka. Hakuwa na mtoto wala mume. Maisha yake yalikuwa ya ulevi.

Nilikumbuka jinsi alivyokataa katakata kusoma tukiwa katika darasa la saba. Alidai kuwa masomo yalijaa mateso mengi mno. Nyumbani kwao pia hakuishi, alitorokea kusikojulikana. Nilikutana naye tena baada ya kukamilisha masomo yangu na kuajiriwa katika kampuni moja ya kuuza magari mjini. Hapo ndipo nilipopatana na Potoka. Alikuwa ameteseka si haba. Kule nyumbani asingerudi kwa kuwa wazazi wake walikuwa **wameaga dunia**.

Potoka alipoijua nyumba yangu, alifanya mazoea ya kunitembelea kila siku na kufurahia mlo nyumbani kwangu. Alisema kuwa chakula hicho kilikuwa kitamu kama asali. Nililazimika kuhamia katika nyumba nyingine wakati Potoka alipoanza kuiba vitu katika nyumba yangu. Kwa kweli, asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Gari lilipofika maegeshoni, nilisubiri kwanza Potoka ashuke ndipo nami nikashuka. Nilisimama kwenye stani hadi nilipohakikisha kuwa ameenda kabisa, ndipo nami nikapiga guu hadi nyumbani.

---

**41.** Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kuwa:
A. mwandishi alitoka kazini kama kawaida kuyakimbiza mambo kadhaa
B. mwandishi alitoka kazini kabla ya alasiri siku za mwisho za mwaka
C. mwandishi hakuwa na sababu hasa ya kumtoa kazini
D. mwandishi hakuwa na la kufanya pale kazini ndipo akaondoka.

**42.** Ni nini ambacho hakikutendeka kabla ya mwandishi kuingia ndani ya matwana?
A. Kusikia sauti ya abiria aliyeongea kwa huzuni na huruma.
B. Wachuuzi kuendeleza kazi zao.
C. Kupishana na magari yaliyokuwa yakipita.
D. Utingo kutangaza magari yao.

**43.** Kwa nini watu walimchangia abiria yule pesa?
A. Walijua kuwa alikuwa katika shida.
B. Walihakikishiwa kuwa alikuwa katika shida.
C. Walidhani kuwa alikuwa katika shida.
D. Walionelea kuwa alikuwa katika shida.

**44.** Ukweli ni kuwa abiria aliyeomba pesa ndani ya gari alikuwa;
A. mjanja B. mzalendo
C. mchochezi D. mwaminifu

**45.** Aya ya tatu inadokeza kuwa abiria wengi walishangaa;
A. walipoambiwa kuwa abiria yule aliitwa Potoka
B. walipogundua kuwa mtu yule hakuwa na uwezo wa kumnunulia mwanawe chakula
C. walipogundua kuwa mwandishi aliijua sauti ya abiria aliyeomba pesa
D. walipomwona abiria aliyewaomba pesa akitoa simu yake na kubofya nambari kadhaa.

**46.** Maneno **'wameaga dunia'** yana maana gani namna yalivyotumiwa katika kifungu?
A. Wametoroka.
B. Wamekuwa maskini.
C. Wamekuwa wagonjwa.
D. Wamekufa.

**47.** **'Usingizi ulianza kunibembeleza ili unifunike gubigubi'**. Maneno haya yanamaanisha kuwa msemaji:
A. alifunikwa kwa blanketi
B. alitamani kulala
C. alibembelezwa
D. alifunika usingizi.

**48.** Kulingana na ufahamu, Potoka;
A. hakuenda shuleni hata kidogo
B. hakumaliza masomo ya shule ya msingi
C. alikuwa na mtoto mchanga nyumbani kwake
D. aliajiriwa katika kampuni ya kuuza magari.

**49.** Methali '**Asiyesikia la mkuu huvunjika guu'** imedhihirika pale ambapo:
A. Potoka aliombaomba pesa ndani ya gari
B. Potoka aliishi karibu na mwandishi
C. Potoka alikataa kusoma kisha akateseka maishani
D. wazazi wa Potoka walishindwa kumpeleka shuleni.

**50.** Yafuatayo ni mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki **isipokuwa**:
A. Elimu ina umuhimu maishani.
B. Mtu mvumilivu hufaidi maishani.
C. Ni vyema kufuata ushauri unaopewa.
D. Uzembe humfaidi mtu wakati fulani.